# MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA MKOA WA IRINGA
## Umetolewa: 27/10/2021

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika mkoa wa Iringa na wilaya zake:

(i) Ngazi ya Mkoa




**Kielelezo 1: (a)** Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 - Aprili, 2022) kwa mkoa wa Iringa. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za Msimu katika sehemu mbalimbali za mkoa wa Iringa.

**Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Novemba hadi Aprili, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine, yamezingatiwa.

### Dondoo

- *Kwa ujumla mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Iringa.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa katika msimu huu.*

### Mvua za Msimu (Novemba, 2021 - Aprili, 2022)

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya Mkoa wa Iringa. Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021 na kuisha wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.

***Angalizo:***
*Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.*

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA WILAYA YA IRINGA
## Umetolewa: 27/10/2021

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Iringa.




Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili, 2022) kwa wilaya ya Iringa, Iringa.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Iringa.*
- *Mvua za msimu zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.*
- *Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora zinazostahimili ukame na kukomaa kwa muda mfupi na mazao mbadala yanayostahimili mvua chache.*

### Mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili 2022) kwa wilaya ya Iringa.

**Zitaanza:** Kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.

**Zitaisha:** Wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Novemba – Aprili kwa Wilaya ya Iringa ni milimita 700 hadi 800.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Machi, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku 10 au zaidi katika msimu huu.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Msimu uliopita.

### Angalizo:

**-Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

**-Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.
- Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao wanaoambatana na upungufu wa mvua wanaweza kujitokeza.
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

#### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na hali ya hewa inayotarajiwa.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA WILAYA YA KILOLO
## Umetolewa: 27/10/2021

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kilolo.




Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili, 2022) kwa wilaya ya Kilolo, Iringa.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kilolo.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.*
- *Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora zinazovumilia ukame na kukomaa kwa muda mfupi pamoja na mazao mbadala yanayostahimili mvua chache*

### Mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili 2022) kwa wilaya ya Kilolo.

**Zitaanza:** Kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.

**Zitaisha:** Wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Novemba – Aprili kwa Wilaya ya Kilolo ni milimita 700 hadi 750.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Machi, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku 10 au zaidi katika msimu huu.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Msimu uliopita.

### Angalizo:

**-Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

**-Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao.
- Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao wanaoambatana na upungufu wa mvua wanaweza kujitokeza
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

#### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na hali ya hewa inayotarajiwa.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.


Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**
*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8.
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz



**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*105A – 09/19*

Taarifa hii Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

(II) Ngazi ya Wilaya

# MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA WILAYA YA MUFINDI
## Umetolewa: 27/10/2021

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Mufindi.




Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili, 2022) kwa wilaya ya Mufindi, Iringa.

## Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Mufindi.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora zinanazovumilia ukame na kukomaa kwa muda mfupi pamoja na mazao mbadala yanayostahimili mvua chache.*

## Mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili 2022) kwa wilaya ya Mufindi.

**Zitaanza:** Kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.

**Zitaisha**: Wiki ya tatu ya mwezi Aprili, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Novemba – Aprili kwa Wilaya ya Mufindi ni milimita 750 hadi 820.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Machi, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku 10 au zaidi katika msimu huu.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Msimu uliopita.

### Angalizo:

**-Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

**-Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

## Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

### Matokeo

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na matunda.
- Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao wanaoambatana na upungufu wa mvua wanaweza kujitokeza.
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.